# HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA TAREHE 20 JULAI, 2024

- **Mheshimiwa Ummy Nderinanga (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu);**

- **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

- **Mheshimiwa Thobias Andengenye, Kamishna Generali wa Zimamoto na Uokoaji (Mstaafu) – Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, pamoja na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa mliopo,**

- **Mheshimiwa Jaji (Rufaa) Jacobs C. M. Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;**

- **Mheshimiwa Jaji George Joseph Kazi, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar;**

- **Mheshimiwa Jaji wa Rufaa (Mst.) Mbarouk Salim Mbarouk, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;**

- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;**

- **Ndugu Ramadhani Kailima, Mkurugenzi wa Uchaguzi - Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;**

- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa;**

- **Waheshimiwa Mabalozi Mnaowakilisha Nchi Mbalimbali;**

- **Waheshimiwa Wabunge wote Mliopo;**

- **Viongozi wa Madhehebu ya Dini;**

- **Wanahabari;**

- **Wageni Waalikwa;**

- **Mabibi na Mabwana.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA!**

**Ndugu Wananchi,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa Kigoma tukiwa na afya njema.

**Pili,** nimpongeze sana Mheshimiwa Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Wajumbe na watendaji wote kwa kukamilisha maandalizi yote muhimu na hatimaye leo tunaanza rasmi zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura baada ya uzinduzi.

**Kipekee**, ninatoa pongezi nyingi kwa uongozi wa Mkoa wa Kigoma ambao ni wenyeji wetu katika uzinduzi huu. Ushiriki na ushirikiano wenu katika maandalizi umeipa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi mwanya wa kupata mafanikio katika uzinduzi na kuhamasisha utayari wa wananchi kushiriki katika zoezi hili muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

## SALAMU ZA VIONGOZI WAKUU WA NCHI

***Ndugu Wananchi,*** naomba nitumie nafsi hii kuwafikishia salamu zenu za heri kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambao wanawatakia kila la heri katika utekelezaji wa zoezi hili muhimu.

Viongozi wetu wote kwa pamoja wamenituma nitoe rai kwa Watanzania kuthamini zoezi hili na kujitokeza kwa wingi kuanzia siku ya leo hadi hapo zoezi litakapohitimishwa kuboresha taarifa au kuhamisha taarifa zao kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo lingine.

**UMUHUMU WA ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA MPIGA KURA**

***Ndugu Wananchi**,* kama mnavyofahamu, zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linaloanza leo ni muhimu sana katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuendeshwa kwa misingi ya kidemokrasia.

Zoezi hili lina lengo la kuhakikisha wananchi wote wenye sifa wanapata na kutumia haki yao ya kikatiba kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Vilevile, umuhimu wa zoezi hili unatokana na ukweli kwamba hii ni hatua muhimu ya maandalizi ya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani

utakaofanyika mwaka 2025 hapa nchini. Pia kutokana na uwepo kundi kubwa la wananchi waliopata sifa ya kiumri tangu uchaguzi uliopita, zoezi hili ni muhimu kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura wapya.

***Ndugu Wananchi**,* Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022; inakadiriwa kuwa jumla ya wapiga kura wapya **5,586,433** wataandikishwa. Hawa ni wale waliotimiza umri wa miaka 18 katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 baada ya uchaguzi mkuu uliopita na ambao watatimiza umri huo ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

***Ndugu Wananchi**,* kwa upande mwingine, takwimu hizo zinaonesha kuwa wengi wanatorajiwa kuandikishwa kuwa wapiga kura wapya ni vijana. Hili ni kundi kubwa na muhimu sana katika mchakato wa uchaguzi.

***Ndugu Wananchi**,* maboresho ya daftari la mpigakura, mbali ya kuandikisha wapiga kura wapya, hii ni fursa muhimu kwa wapiga

kura ambao kwa sababu moja au nyingine kadi zao za mpiga kura zimepotea au kuharibika au wamehama kutoka eneo moja kwenda jingine la uchaguzi, kufika kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura ili kuboresha taarifa zao na kupatiwa kadi mpya itakayowawezesha kupiga kura.

***Ndugu Wananchi***, kwa mujibu wa taarifa za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, inakadiriwa kuwa wapiga kura **4,369,531** wataboresha taarifa zao. Idadi hii siyo ndogo kwenye zoezi la kupiga kura. Hivyo, nitoe rai kwa kila mpiga kura aliyeandikishwa mwenye uhitaji wa kuboresha taarifa iwe kwa kurekebisha taarifa au kuhama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine asisite kufika katika kituo cha kuandikisha kwani Tume imeshajipanga ili kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa.

**PONGEZI KWA TUME KWA MAANDALIZI YA UCHAGUZI MKUU WA 2025**

***Ndugu Wananchi***, nimefarijika sana kwa hatua ambazo zimekuwa zikichuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ikiwemo

kuhakikisha mawanda ya kuwafikia wapiga kura wote yanapanuliwa.

**Maboresho ya mifumo**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imefanya **maboresho ya mifumo ambayo yanawezesha** wapiga kura waliomo kwenye Daftari la Mpiga Kura kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao. Kupitia mfumo huo wapiga kura wataweza kurekebisha taarifa zao binafsi au kuhama kituo kimoja cha kupigia kura kwenda kingine kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu janja au Kompyuta.

***Ndugu Wananchi***, hii ni hatua kubwa sana ya mafanikio ambayo itaondoa changamoto ya kuogopa foleni. Mfumo huo wa kidijitali ni fursa nzuri iliyopo nchini kwetu, sote tuitumie vema kwani itapunguza msongamano wakati wa kuboresha Daftari, kuokoa muda na kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli za ujenzi wa Taifa. Kwa maneno mengine mfumo huo utaongeza ufanisi zaidi katika utoaji wa huduma.

**Hongereni sana** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kusanifu na kuanzisha mfumo huu saidizi ambao utasaidia sana kuleta ufanisi katika zoezi la uboreshaji wa daftari la wapiga kura.

**Kuongeza Idadi ya Vituo**

***Ndugu Wananchi***, eneo lingine ni nyongeza ya vituo **2,312** vya kuandikisha wapiga kura katika mwaka 2024/2025. Nyongeza hiyo inafanya idadi ya vituo kufikia **40,126**. Kwa upande mwingine vituo vya wapiga kura vimesogezwa karibu zaidi na wananchi wote katika maeneo ya uandikishwaji ambayo ni mitaa, vijiji, shehia na vitongoji katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Ndugu Wananchi***, licha ya hayo vipo vituo vingine vipya **130** ambavyo vitatumika kuandikisha wafungwa wanaotumikia vifungo ambavyo ni chini ya miezi sita na mahabusu katika magereza ya Tanzania Bara. Vilevile, vituo **10** vipya kwenye vyuo vya mafunzo vitakavyotumika kuandikisha wanaotumikia vifungo chini ya miezi sita na mahabusu kwa Tanzania Zanzibar.

***Ndugu Wananchi****,* ninaipongeza sana Tume Huru ya Taifa Uchaguzi kwa hatua hii muhimu kwani hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu fursa kutolewa kwa wafungwa wanaotumikia vifungo vya chini ya miezi sita gerezani au kwenye vyuo vya mafunzo na mahabusu kujiandikisha kuwa wapiga kura.

***Ndugu Wananchi****,* kwa kuwa suala hilo ni jipya, katika utekelezaji wa jukumu hilo, Tume wakati wote izingatie matakwa na masharti ya Sheria na taratibu zinazosimamia magereza na vyuo vya mafunzo sambamba na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024. Mazingatio hayo yatasaidia kuepusha migongano na katika hili ni lazima yawepo mashauriano ya mara kwa mara wakati wote wa utekelezaji wa suala hili baina ya Tume na vyombo husika.

**WAJIBU WA RAIA NA ASASI NA TAASISI KUELEKEA UCHAGUZI MKUU**

***Ndugu Wananchi*** nitumie nafsi hii sasa kueleza kwa kifupi kuhusu wajibu wa kila mwananchi katika kufanikisha mchakato kuelekea Uchaguzi Mkuu kama ifuatavyo:

**Wajibu wa kila Mtanzania**

***Ndugu Wananchi,*** kila Mtanzania ashiriki katika usimamizi wa suala hili kwani wanaotakiwa kuandikishwa ni raia wa Tanzania tu wenye sifa zilizobainishwa kwa mujibu wa sheria. Wananchi ni watambuzi wa kwanza, niwasihi sana tuwe wazalendo, huu ni wajibu wa raia wa Tanzania kuhakikisha wanaoandikishwa ni Watanzania tu.

Kadhalika, ni wajibu wetu sisi sote Watanzania kutumia nafasi hii kulikagua Daftari la Awali litakapowekwa wazi na kutoa taarifa iwapo kuna watu, ambao tunadhani hawana sifa kama vile wasio raia wa Tanzania na tayari kwa bahati mbaya wameshaandikishwa, ili waweze kuondolewa kwenye Daftari kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

**Jeshi la Magereza na upande wa Zanzibar vyuo vya mafunzo**

***Ndugu Wananchi****,* ili kufanikisha zoezi la kuandikisha wafungwa wanaotumikia vifungo vya chini ya miezi sita gerezani au kwenye vyuo vya mafunzo na mahabusu kujiandikisha, Jeshi la Magereza na upande wa Zanzibar vyuo vya mafunzo wanawajibika kuweka miundombinu wezeshi ili Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi iweze kutekeleza wajibu huo kwa ufanisi.

Aidha, Jeshi la Uhamiaji liwajibike kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuwatambua na kutoa taarifa za uwepo wa mtu au watu ambao siyo raia wa Tanzania, walioandikishwa tayari au wanaopanga kwenda kuandikishwa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa mapema dhidi yao.

**Wajibu wa vyama vya Siasa**

***Ndugu wananchi*****,** kwa kuwa vyama vya siasa vinayo fursa ya kisheria kuweka mawakala wa uandikishaji kwenye kila kituo cha uandikishaji chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, ninatoa rai kwa viongozi wa vyama vya siasa kuhakikisha mawakala wao wanatoka kwenye mtaa, kijiji na shehia husika ili waweze kutimiza wajibu wao

wa kisheria wa kuwatambua watu wenye sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura. Iwapo hili litafanyika ipasavyo, uwezekanao wa kuandikisha wapiga kura ambao siyo raia wa Tanzania halitakuwepo.

**Mawakala wa Vyama vya Siasa**

***Ndugu wananchi*****,** kwa upande wa mawakala watakaoteuliwa na vyama vya siasa nao wanaowajibu wa kutambua wenye sifa za kuandikishwa wanaofika kwenye kituo kwa ajili ya kuandikishwa kuwa wapigakura. Niwasisitize mawakala wote wawe wazalendo, lakini pia wawe na imani na chombo kilichopewa jukumu la kusimamia zoezi hilo hapa nchini.

Vilevile, mawakala wanawajibika kutoa taarifa iwapo changamoto zitajitokeza kwa Afisa Mwandikishaji au kwa Viongozi wa Tume ili hatua stahiki zichukuliwe badala ya kuwasilisha kwenye vyombo au kwenye mamlaka zisizohusika.

**Watendaji walioteuliwa na Tume**

***Ndugu wananchi*****,** ninawasii sana watendaji walioteuliwa na Tume kuanzia ngazi ya mkoa, jimbo, kata na kituo cha kuandikisha wapiga kura kuwa waadilifu na watangulize uzalendo kwa kutotoa fursa kwa watu ambao hawana sifa za kushiriki katika uboreshaji. Kila mmoja ajitume, afanye kazi kwa weledi na kutumia lugha nzuri wakati wote wa utekelezaji wa majukumu aliyopangiwa. Masuala hayo yatekelezwe sambamba na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo itakayotolewa na Tume, ili kufanikisha zoezi hili muhimu kwa Kitaifa.

***Ndugu Wananchi,*** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, inawajibika kuchukua hatua za haraka za kuwaondoa watendaji watakapobainika kufanya jambo linalokwenda kinyume na sheria. Hatua za haraka ziendelee kuchukuliwa ili kujenga imani ya wadau wa uchaguzi katika zoezi ambalo Tume inalianza leo.

**Taasisi na Asasi za kiraia**

***Ndugu wananchi,*** eneo lingine muhimu ni suala la utoaji wa elimu ya mpigakura. Katika eneo hili taasisi na asasi zote zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura na zile zilizokubaliwa kuwa Waangalizi wakati wa zoezi hili la uboreshaji, zihakikishe

zinatekeleza kazi zao kwa kuzingatia masharti ya vibali na miongozo iliyotolewa na itakayotolewa na Tume.

***Ndugu Wananchi,*** kwa upande mwingine taasisi na asasi za kiraia zinapaswa kutambua uwepo wa sheria nyingine za nchi. Sheria hizo zinaendelea kufanya kazi na kibali kisiwe kisingizio cha ukiukwaji wa sheria zingine kwa namna yoyote ile. Ni vema wakati wote ziepuke kufanya masuala ambayo hayamo kwenye miongozo waliyopewa kwa mujibu wa vibali vyao.

***Ndugu wananchi*****,** ninazipongeza Taasisi na Asasi zilizopewa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura. Serikali kwa upande wake ina matumaini makubwa ya kwamba wananchi wengi zaidi watapata elimu kuhusu uboreshaji wa Daftari, watahamasika na kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kuwa wapiga kura au kuboresha au kuhamisha taarifa zao.

**Vyombo vya Habari**

***Ndugu Wananchi,*** vyombo vya habari vinayo dhima ya kutoa habari sahihi, za kweli na kwa wakati kuhusu zoezi hili. Pia

mnaowajibu kwa kutumia kalamu zenu, kuwakumbusha wadau wa uboreshaji kutumia taratibu zilizoainishwa kwenye sheria, kanuni na miongozo kutatua au kuwasilisha malalamiko iwapo kutajitokeza changamoto ya aina yoyote wakati wa uendeshaji wa zoezi hili. Aidha, unapotokea upotoshaji wa aina yoyote, vyombo vya habari viwe vya kwanza kupaza sauti ili kuonesha upotoshwaji huo.

***Ndugu Wananchi,*** kama mnavyofahamu vyama vya siasa ni wadau wakuu katika zoezi hili. Wadau hawa muhimu wanatarajia vyombo vya habari vitoe taarifa zitakazoviwezesha vyama vya siasa kuhamasisha wanachama wao kujitokeza kujiandikisha na kuvifanya vyama ama viafiki na kukubali uendeshaji wa zoezi au kuanza kujenga mashaka na hofu ya uendeshwaji wa zoezi hili.

**MIKAKATI YA SERIKALI KUFANIKISHA UCHAGUZI**

***Ndugu Wananchi,*** Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

inafanikisha jukumu hili kubwa la Kitaifa**.** Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuidhinisha fedha ili Tume itekeleze majukumu yake likiwemo hili la uboreshaji wa Daftari la Wapigakura.

***Ndugu Wananchi,*** zoezi hili la uboreshaji wa Daftari linaloanza leo, litagharimu fedha takriban shilingi **bilioni 418.264.** Fedha hizo zote zinatolewa na Serikali ya awamu ya sita bila kutegemea fedha za kutoka kwa wafadhili. Hadi sasa Serikali imeshaipatia Tume kiasi cha shilingi **bilioni 223.72** ambazo zimetumika kununua vifaa na matumizi mengine muhimu katika zoezi la uboreshaji.

***Ndugu Wananchi,*** baadhi ya shughuli zilizofanywa na Tume ni pamoja na kununua BVR Kits mpya **6,000** zinazotumia mfumo endeshi wa kisasa wa *android*, kununua magari mpya **25 na** kuchapa fomu zote zitakazotumika kwenye zoezi hili. Kadhalika, kuajiri watumishi wa muda **492,** kulipa gharama za watendaji **64,068** walioteuliwa kutekeleza majukumu haya,

kuhuisha mifumo ya uandikishaji na kufanya ukarabati wa majengo ya Tume.

***Ndugu Wananchi***, niwahakikishie Watanzania wote kuwa, Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amedhamiria kuhakikisha kuwa Uchaguzi unakuwa wa Haki, Huru na Serikali kugharamia shughuli zote zinazohusiana na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025 kwa fedha zake za ndani. Upo msemo wa Kiswahili "**bure ghali**" kwa kuzingatia ukweli huo Serikali itaendelea kufanya kila jitihada ili Tume iendelee kufanya kazi kwa uhuru na kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**MAENEO YA MSISITIZO**

***Ndugu Wananchi****,* nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu ninaomba sasa nitumie nafasi hii kuweka msisitizo katika mauala muhimu kama ifuatavyo:

**Moja:** Watanzania wote wenye sifa za kujiandikisha au kurekebisha taarifa au kuhamisha taarifa zao mjitokeze kwa wingi ili kuwa na uhakika wa kupiga kura wakati wa uchaguzi mkuu unaokuja. Tumieni fursa ya ongezeko la vituo kujitokeza kwa wingi kwa wale wanaondikishwa upya au wanaoboresha taarifa na kuhamisha taarifa zao au waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika.

**Mbili:** Vijana waliofikia umri wa kupiga kura shime, tumieni fursa ya uboreshaji kujiandikisha kuwa wapiga kura ili wakati wa uchaguzi ukifika mtumie haki hiyo kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Tatu:** Jeshi la Polisi nchini kuhakikisha linaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote ambayo zoezi hili linafanyika na kwa kuanzia katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, epukeni matumizi ya nguvu kupita kiasi zinazoweza kuhatarisha usalama kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura.

**Nne:** Vyombo vya habari, sambamba na pongezi kwa kazi nzuri na muhimu ya kuuhabarisha umma tangu hatua za mwanzo za maandalizi ya zoezi hili linaloanza leo, niwasisitize endeleeni kutoa habari sahihi na zilizofanyiwa utafiti kuhusu zoezi hili muhimu kwa nchi yetu.

**Tano:** Wazee wa kimila, ninawasihi sana tumieni ushawishi wenu katika jamii, kuwahimiza watu wenye sifa kwenye jamii mnazoziongoza, wajiandikishe kuwa wapiga kura au kuboresha taarifa zao ili ifikapo mwaka 2025 waweze kupiga kura ya kumchangua Rais, Mbunge na Diwani.

**Sita:** Viongozi wa dini tumieni majukwaa ya misikiti na makanisa kuwahimiza na kuwakumbusha waamini na waumini wenu wajitokeze kujiandikisha kuwa wapiga kura. Vilevile, endeleeni kuhamasisha waumini wenu waliopoteza kadi au kadi zao zimeharibika pamoja na wale wanaotaka kuboresha taarifa zao binafsi au kuhama kituo kwa pamoja watumie muda huu kwenda kwenye

vituo kwa ajili ya kuboresha taarifa zao na kukamilisha taratibu zilizowekwa.

***Ndugu Wananchi***, kupitia ushiriki wa wadau mbalimbali nina hakika kuwa Tume itaweza kufikia lengo ililojiwekea la kuwa na wapiga kura **34,746,638.** Serikali itaendelea kuhakikisha mazingira mazuri kwa wananchi kujitokeza kwa wingi na kutumia vema muda wa siku saba zitakazotumika kwa kila kituo cha kuandikisha wapiga kura.

## HITIMISHO

***Ndugu Wananchi****, mwisho kabisa,* nirudie kuwasihi wananchi wa mikoa ambayo zoezi la uboreshaji linaanza kwa mzunguko wa kwanza, yaani mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora, kujitokeza wa wingi. Tume imechagua kuanza na mikoa yenu hivyo tumieni first hii kujitokeza kwa wingi kuandikishwa kuwa wapiga kura. Jitokezeni kwa wingi kwenye vituo kuanzia leo tarehe 20 Julai, 2024 hadi tarehe 26 Julai, 2024 ambayo ni kilele cha zoezi hilo.

***Ndugu Wananchi****,* nitumie fursa hii kutoa wito kwa mikoa inayofuata ambayo ni Geita na Kagera, kisha Mwanza, Shinyanga

na baadae Mara, Simiyu na sehemu ya Mkoa wa Manyara, jiandaeni ili tarehe ikifika mjitokeze kwa wingi kutimiza haki yenu ya kujiandikisha ama kuboresha au kuhamisha taarifa zenu.

Baada ya kusema hayo, sasa **nipo tayari kufanya uzinduzi rasmi wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya kwanza leo tarehe 20 Julai, 2024 hapa Mkoani Kigoma.**

**Ahsanteni kwa kunisikiliza!**